JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Dodoma*
*22 Septemba, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA
# SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mama Fatma Karume, mjane wa Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Dkt. Samia anatoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Zanzibar; familia, ndugu, jamaa na wananchi wote wa Zanzibar kwa msiba huo. Aidha, anawaombea wafiwa wote subira na faraja katika kipindi hiki cha majonzi.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amin.

***Inna lillahi waina ilayhi raajiun!***

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu